# MTIHANI WA MWIGO WA LANJET

**MUHULA WA PILI 2022**

**102/2 KARATASI YA PILI**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA**

## UFAHAMU

a) i) Kuvuruga/ kuharibu hali ya maisha ya watu. ***(alama 1)***

ii) Kuwaua watu ***(alama 1)***

b) i)Ugonjwa uletwao na kula chakula kichafu.Dalili zake ni kuendesha,kuumwa na tumbo na homa kali. ***(alama 1)***

ii) Tibii, ugonjwa wa kukohoa damu ***(alama 1)***

c) Kutokana na kasi yake ya kuua watu ***(alama 1)***

d)- Huambukizwa sana kwa watu walio na miaka kati yawalio na nguvu za kutunza jamii/ watasalia wakongwe na watoto wasioweza kujimudu.

- Umesababisha vifo vingi

- Hospitali na zahanati zimeshindwa kukidhi mahitaji ya wagonjwa.***(hoja 3 x 1 = 3)***

e) - Maradhi haya sasa yamekuwa janga la kitaifa

- Makundi ya kujitolea na mashirika mbalimbali yameundwa ili kuwahudumia wagonjwa

- Wagonjwa wengi pia huishia kutibiwa nyumbani

- Wanasayansi na madaktari wanatafuta tiba ***(Hoja 4 x ½ = 2)***

f) - Tuwe na matumaini kwamba siku moja tiba itapatikana

- Tujikinge kutokana na maradhi haya

- Tuwe na subira kwani subira huvuta heri *(hoja 3 x 1 = 3)*

g) i) Utaratibu wa utendaji au utekelezaji ***(alama 1)***

ii) Wema /baraka/ fanaka/ ustawi ***(alama 1)***

**<u>Maelezo ya kutuza</u>**

- Makosa ya tahajia – Ondoa nusu 6 yaani ½ x 6

ili kuwa jumla ya alama 3

- Makosa ya sarufi – Usiondoe zaidi ya nusu ya tuzo kwa kila swali.

**2.UFUPISHO (ALAMA 15)**

(a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi? (alama 7, 1 utiririko)

- ***Tunapinga na kulaani visa vya ugaidi.***
- ***Ugaidi ni kitendo cha kinyama kinachotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu.***
- ***Ugaidi hauna uhusiano na dini yoyote.***
- ***Polisi wanazembea katika kuzuia matendo ya kigaidi.***
- ***Polisi wabuni njia mbadala ya kukabiliana na ugaidi badala ya kunasa raia wasio na hatia.***
- ***Wakenya wasio na makosa huteswa na kuuawa kinyama.***
- ***Magaidi watalipia matendo yao.***
- ***Wakenya wana haki ya kulindwa kikatiba.***

*Hoja zozote 7×1=7, alama 1 ya utiririko.*

(b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50, fupisha aya mbili za mwisho. (alama 6, 1 utiririko)

- ***Raia wasio na hatia hunaswa.***
- ***Hurundikwa kwenye seli na kuachiliwa huru kama wameteseka.***
- ***Huu ni ukiukaji wa haki za binadamu.***
- ***Hii ni hila ya polisi kujionyesha kuwa wanafanya kazi.***
- ***Magaidi huendeleza shughuli zao.***
- ***Polisi wanapaswa kubuni njia zitakazowapa mwelekeo mwafaka kuhusu wahalifu.***
- ***Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo.***
- ***Maafisa wa usalama kupata habari muhimu kutoka kwa raia.***

*Hoja zozote 6×1=1, alama 1 ya utiririko.*

*Ondoa ½ alama kwa kila kosa la sarufi hadi makosa sita kila litokeapo mara ya kwanza.*

*Ondoa ½ alama kwa kila kosa la hijai hadi makosa sita kila litokeapo mara ya kwanza.*

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) (i) Kipashio kikubwa zaidi katika ujenzi wa lugha kinaitwaje? (alama 1)

- *Sentensi*

(b) Andika sauti mbili ambazo ni vikwamizo vya mdomo wa meno. (alama 2)

- */f/ na /v/*

(a) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Nitawafundisha usemi wa taarifa kesho," mwalimu alituambia.

- *Mwalimu alituambia kuwa angetufundisha usemi wa taarifa siku ambayo ingefuata (keshoye)*

(b) Tunga sentensi moja ukitumia kielezi cha nomino. (alama 2)




(c) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (alama 4)

Wanafunzi wenye bidii masomoni hufuzu mtihani.

- *Kitondo/ambiwa – baba*
- *Kipozi/yamba tenda – habari*

(d) Tambua muundo wa virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo: (alama 2)

- *Nomino na kishazi tegemezi*

(ii) Mara nyingine msimu wa umewadia

- *Kwelezi la idadi*

(e) Andika upya sentensi zifuatazo kwa kuzingatia kauli zilizomo mabanoni. (alama 2)

(i) Watoto wenyewe wamekunywa maziwa yao yote. (tendwa)

- *Maziwa yote ya watoto yamenyweka nao wenyewe*

(ii) Pombe haramu inawafisha Wakenya wengi. (Badilisha kitenzi kiwe nomino)

- *Pombe haramu imesababisha vifo vya wakenya wengi*

(f) Kanusha kwa wingi

- *Uovu waliotuonyesha*
- *Maoni waliyotuonyesha*

(g) Tunga sentensi mbili tofauti kuonyesha matumizi yafuatayo ya ndivyo. (alama 2)

(a) Jinsi

- *Hivi ndivyo aandikavyo*

(b) Kirejeshi cha kuthibitisha.

- *Hivi ndivyo vilivyorumbiwa jana*

(h) Eleza maana tatu zinazoibuliwa na vitate vilivyotumika katika sentensi hii. (alama 3)

Bosi wetu ana pozi nyingi lakini ni bozi sana.

- *Bosi – mkubwa wa ofisi/ikawa Fulani/mwajiri /tarjiri*
- *Pozi – maringo (mtwazo), madaha, matuko, gogi, majivuno, goto*
- *Bozi – mpubmavu bahau, fala, bwege, zebe, bakunja, mjinga*

(i) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.

Uso wa kijana Yule ulichujuka alipoanguka. (alama 2)

- *Juso la jana lile lilichujuka lilipoanguka*
- *Jijusa la jijana lile lilichunyika*

(j) Eleza matumizi mawili ya viakifishi vifuatavyo: (alama 4)

**i. Herufi nzito (H) / zilizokolewa.**

- *Kuonysha wanwani, mada k.m utangulizi, sura ya pili, vishozi*
- *Kusisitiza kitulia mazo km wakihishi vya nafasi ni mimi , wewe*

- *Madekezo k.m kwa mfano*

(ii) **Mstari**

- *Kutilia neon au fungu la maneno msisitizo*
- *Kuonyesho anwani ya vitabu na majin aya majarida, magazeti km gazeti la taifa leo, riwaya ya kidagaa kimemzoea*

Bainisha mofimu za: (alama 3)

Nitakujia

- *Ni – nafsi*
- *Ta – wakati*
- *Ku – nafsi/mtendewa/yambiwa*

(k) Unganisha sentensi hizi kwa kutumia kirejeshi cha kati mwafaka. (alama 1)

Gari limeibwa. Gari ni langu.

- *Gari lililoibwa ni langu*

(l) Ainisha vihusishi katika sentensi hizi: (alama 2)

(i) Mwanafunzi huyu ni mwerevy sana kuliko wenzake wote.

- *Kuliko – ulinganisho*

(ii) Tangu apate mamlaka amepuuzxa wadogo wake.

- *Tangu – uhusiano wa wakati*

(m) Unda kitenzi kutokana na neon "Zawadi" (alama 1)

- *Zawadi, zawidia, zawidika, zawidiano n.k*

(n) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Ingawa amefunga bao hajacheza kwa muda.

- *Ingawa amefunga bao – kishazi tegemezi*
- *Hajacheza kwa muda – kishazi huru*

**4. ISIMU JAMII**

**" Maafisa 3 wakana kusaidia mshukiwa wa mauwaji ya watoto kutoroka kituoni.**

Maafisa watatu wa polisi jana walikana mashtaka ya kumsaidia mshukiwa wa mauaji ya watoto 13 kutoroka kutoka kituo cha polisi…"

(a) Huku ukitoa sababu mbili, tambua sajili hii. ( alama 3)

***Sajili ya magazetini/ matangazo***

***Sababu – kuwepo kwa anwani/mada yenye mvuto***

***- matumizi ya usemi wa taarifa/ lugha ya kuripoti*** ***( sajili 1, sifa 2x1)***

(b) Fafanua sifa zozote nyingine saba za sajili hii. (alama 7)

***i) mara nyingi vichwa vya habari havizingatii sarufi – ili kuokoa nafasi katika gazeti/muda***

***ii) baadhi ya jumbe ya mambo ya kweli – ili*** *kuvutia* ***wasomaji/ wanunuzi/wasikilizaji/mtazamaji***

***iii) mada/ anwani huwa fupi sana nay a kuvutia- ili kuvutia wateja/ wasomaji wa gazeti/wasikilizaji***

***iv) lugha inayotumika hutegemea taarifa inayotolewa- kila taaluma ina msamiati wake.***

***v) ujumbe huandikwa/husomwa katika aya fupifupi/ kwa muhtasari- ili kuokoa nafasi katika magazeti/muda***

***Vi) lugha yenye kauli/ sentensi ndefundefu- ili kufafanua hoja kikamilifu.***

***vii) matumizi ya tarakimu badala ya maneno- ili kuokoa nafasi/kusomeka haraka***

***viii) lugha ya kuvutia – "mwalimu aonja asali"***

***ix) matumizi mengi ya chuku- " paka amla ndovu"***

***x) matumizi ya sitiari/jazanda- ili kutasfidi lugha***

***xi) matumizi ya lugha rahisi- ili kupasha ujumbe kwa watu wa matabaka yote.***

***xii) lugha ya maelezo – ili kupasha ujumbe kwa njia nyepese na kueleweka rahisi.*** ***(zozote 7x1)***

***xiii) matumizi ya tasfida – ili kuficha ukali***

***xiv) lugha ya picha / michoro – ili ujumbe ueleweke***